# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI

## MUHTASARI WA MAFUNZO YA UALIMU WA ELIMU KWA MICHEZO NGAZI YA CHETI

## USIMAMIZI NA USALAMA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO

**2009**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, 2009

ISBN …………………………………….

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kutoa, kunakili au kuchapisha kwa namna yoyote muhtasari huu bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Imetolewa na:

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar -es- Salaam
Tanzania

Simu: +255 222 773006, 2774420
Nukushi: +255 222 774420
Barua pepe: director.tie@tie.go.tz

## IDHINI

Mafunzo ya Ualimu wa Elimu ya Msingi Ngazi ya Cheti ni ya miaka miwili na yamekusudiwa kuandaa walimu mahiri wenye uwezo wa kufanya kazi kwa dhati. Walimu hao watafundisha katika shule za msingi. Mwalimu mwanafunzi atatambuliwa kuwa ni mwalimu baada ya kuhudhuria na kufaulu mafunzo ya cheti ya miaka miwili ambamo pia atafanya na kufaulu mazoezi ya kufundisha.

Andiko hili linaidhinishwa kuwa ni **Muhasari wa Taaluma na Utaalam wa Somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo kwa Kozi ya Ualimu Elimu kwa Michezo, Ngazi ya Cheti** wa mwaka 2009

Umeidhinishwa na .....................................................

Saini...............................................................................

Tarehe...................................................................2009

**Kamishna wa Elimu**
**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi**
**S.L.P. 9121**
**DAR -ES -SALAAM**

**Simu: +255 222 110150, 1101799, 11046**
**Nukushi: + 255 222 11 3271**
**Tovuti: www.moe.go.tz**

## YALIYOMO

IDHINI....................................................................................................ii
Utangulizi ..............................................................................................iv
Sababu za Kuwa na Muhtasari Huu ....................................................................iv
Madhumuni ya Kufundisha Somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo ..............................................................................................................iv
Ujuzi wa Somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo ..........................v
Malengo ya somo la Usimamizi na Usalama katika Michezo ......................................v
Muundo wa Muhtasari.......................................................................................v
Upimaji na Tathmini ya Maendeleo ya Mwanachuo .................................................vi
Muda wa mafunzo.............................................................................................vi
1.0 UTAWALA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO ...................................................1
1.1 Dhana ya Utawala ...........................................................................................1
1.2 Uandaaji na Usimamizi wa Shughuli za Elimu kwa Michezo ..............................2
1.3 Kuwajibika Kisheria katika Michezo ..................................................................2
2.0 MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO .............4
2.1 Mawasiliano katika Michezo..............................................................................4
2.2 Vyombo vya Habari na Elimu kwa Michezo .......................................................5
2.3 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu kwa Michezo.......................5
3.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI KATIKA ELIMU KWA MICHEZO ......................7
3.1 Rasilimali katika Michezo...................................................................................7
3.2 Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Michezo ....................................................8
3.3 Kujitolea katika shughuli za Elimu ya michezo ...................................................8
4.0 KUANDAA SHUGHULI ZA ELIMU KWA MICHEZO ........................................10
4.1 Mashindano ......................................................................................................10
4.2 Udhamini na Ufadhili katika Elimu kwa michezo ..............................................11
4.3 Ziara za Kimichezo............................................................................................11
5.0 USALAMA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO ..................................................13
5.1 Usalama wa Vifaa na Mazingira ya Michezo .....................................................13
5.2 Usalama wa Washiriki katika Michezo ..............................................................14
5.3 Magonjwa katika Michezo .................................................................................14
5.4 Michezo na Ukimwi...........................................................................................15
6.0 AJALI KATIKA ELIMU KWA MICHEZO ..........................................................17
6.1 Huduma ya Kwanza...........................................................................................17
6.2 Utoaji wa Huduma ya Kwanza katika Michezo ..................................................17
6.3 Mazoezi kwa Majeruhi.......................................................................................18
6.4 Matumizi ya Madawa Katika Michezo ...............................................................19
VITABU VYA REJEA .............................................................................................21

## Utangulizi

Huu ni muhtasari wa somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo.Hili ni somo jipya lililoanzishwa katika mtaala wa mafunzo Ualimu Ngazi ya Cheti, Elimu kwa Michezo.

Katika somo hili, mwanachuo atapata maarifa na stadi za msingi za kuandaa na kusimamia, kuchukua tahadahri za kuepusha ajali zinazojitokeza katika shughuli za michezo na kutoa huduma ya kwanza.

## Sababu za Kuwa na Muhtasari Huu

Kuanzishwa kwa muhtasari huu unatokana na uamuzi wa serikali wa mwaka 2007 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu katika nyanja ya Elimu kwa michezo pamoja na uamuzi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 2008 wa kuimarisha mafunzo ya ualimu na kutatua tatizo la upungufu wa walimu ngazi ya cheti linalokabili nchi kwa ujumla. Hii ni pamoja na kukidhi mahitaji na idadi ya walimu wa Elimu kwa michezo kutokana na kupanuka kwa sekta ya elimu ya msingi kufuatia kutekelezwa kwa mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), kuongezeka kwa mahitaji ya walimu wenye kiwango cha juu cha taaluma ya Elimu kwa michezo na utaalam na kushughulikia masuala mtambuko.

## Madhumuni ya Kufundisha Somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo

Mafunzo ya Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa michezo yana madhumuni yafuatayo:

a) Kumwezesha mwanachuo kupata maarifa na mbinu za uandaaji, usimamizi, kinga na usalama katika shughuli za Michezo .
b) Kumwezesha mwanachuo kupata maarifa na ujuzi wa kusimamia raslimaliwatu, vitu na fedha katika shughuli za Elimu kwa Michezo na Michezo kwa jumla katika shule za msingi.

**Ujuzi wa Somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo**

Baada ya miaka miwili ya mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti, mwanachuo aweze kuonesha ujuzi katika:

a) Kutawala na kusimamia shughuli za Elimu kwa Michezo na Michezo
b) Kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kwa ufasaha katika shughuli za Elimu kwa Michezo kwa wanafunzi.
c) Kuandaa na kufanya tathmini ya shughuli za michezo
d) Kujenga mahusiano mema na wadau mbalimbali wa michezo.
e) Kutoa huduma ya kwanza kwa kuzingatia kanuni za afya katika michezo.
f) Kuchukua tahadhari za kinga ya ajali na kuzingatia usalama katika michezo.

**Malengo ya somo la Usimamizi na Usalama katika Michezo**

Baada ya mafunzo ya miaka miwili ya ualimu ngazi ya cheti ualimu Elimu kwa Michezo mwanachuo aweze:

a) Kujenga uwezo wa kuandaa na kusimamia shughuli za Elimu kwa Michezo na Michezo.
b) Kujenga uwezo wa kuandaa na kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika Elimu kwa Micheza.
c) Kujenga uelewa na kutumia kanuni za afya, usalama na kinga katika Elimu kwa michezo.

**Muundo wa Muhtasari**

Muhtasari huu wa Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo umebeba mada za utawala, usimamizi na kinga katika michezo. Muhtasari umeundwa kwa kufuata mtiririko wa mada, mada ndogo muda, malengo mahsusi mapendekezo ya mbinu za kufundishia zana za kufundishia na zana za upimaji. Mkufunzi unashauriwa kuwa mbunifu katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji ili kufikia lengo lililokusudiwa.

**Upimaji na Tathmini ya Maendeleo ya Mwanachuo**

Muhtasari huu unatoa mapendekezo ya mbinu za upimaji ambazo zitamwezesha mkufunzi kupima maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji. Mwanachuo atapimwa kwa kutumia mbinu mbalimbali kwa mfano uwasilishaji wa darasani, mkoba wa kazi, kazi binafsi, majaribio na mitihani ya mwisho wa muhula. Upimaji endelezi utakuwa na jumla ya alama 50%.Upimaji tamati utafanyika mwisho wa mafunzo, na utatolewa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA).

**Jedwali la Upimaji Endelezi**

| | **Mbinu za Upimaji** | **Mrudiano** | **Alama** |
|---|---|---|---|
| 1. | Majaribio | 4 | 05 |
| **2.** | Uwasilishaji | 4 | 05 |
| 3. | Kazi mradi | 2 | 10 |
| 4. | Kazi binafsi | 3 | 10 |
| 5. | Mitihani ya muhula | 3 | 20 |
| | | | 50% |

**Muda wa mafunzo**

Mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti Elimu kwa Michezo ni miaka miwili.Somo la Usimamizi na Usalama katika Elimu kwa Michezo lina vipindi viwili kwa wiki na muda wa kila kipindi ni saa moja. Mkufunzi anapaswa azingatie muda uliopangwa ili kuhakikisha wanachuo wanajifunza mada zote.

# 1.0 UTAWALA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO

## 1.1 Dhana ya Utawala

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana na aina za utawala.
b) Kueleza umuhimu wa utawala na usimamizi katika Elimu kwa Michezo
c) Kubainisha misingi ya utawala katika Elimu kwa Michezo.
d) Kutumia misingi ya utawala katika uandaaji na usimamizi wa shughuli za Elimu kwa Michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Igizo dhima
c) Majadiliano katika vikundi

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu mbalimbali na majarida ya kufundishia mada ya Usimamizi na Utawala.
b) Chati mbalimbali za Uongozi na Utawala katika michezo mfano: Wilaya, Mkoa, Taifa, UMITASHUMTA, UMISETA, UMISAVUTA.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Uandishi wa insha.

## 1.2 Uandaaji na Usimamizi wa Shughuli za Elimu kwa Michezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubaini vipengele vya maandalizi ya shughuli za Elimu kwa Michezo.
b) Kuandaa na kusimamia shughuli za Elimu kwa Michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano kwa vikundi.
b) Mazoezi kwa vitendo.
c) Kisa mafunzo kuhusu.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Majarida.
b) Chati yenye vipengele muhimu vya Uandaaji wa Shughuli za  Michezo.
c) Vitabu vya utawala na uongozi wa michezo.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Kazi binafsi.
c) Insha.

## 1.3 Kuwajibika Kisheria katika Michezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na uzembe katika uandaaji na usimamizi wa shughuli za michezo.
b) Kudhibiti madhara yanayoweza kujitokeza katika uandaaji na usimamizi wa shughuli za michezo.

c) Kubainisha uwajibikaji kisheria kutokana na uzembe katika uandaaji na usimamizi wa shughuli za michezo.
d) Kutumia sheria dhidi ya uzembe katika uandaaji na usimamizi wa shughuli za michezo.

**Mbinu za Kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Kisa mafunzo.
d) Igizo dhima.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu na majarida yanayohusu kuwajibika kisheria katika michezo.
b) Mfano wa hati za bima kwa wachezaji.
c) Kisanduku cha Huduma ya kwanza.
d) Vifaa vya kujikinga na madhara katika michezo mbalimbali mfano glovu, kilinda ugoko na bandeji.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Insha.
c) Orodha hakiki.
d) Jaribio.

## 2.0 MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO

### 2.1 Mawasiliano katika Michezo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana, aina na umuhimu wa mawasiliano katika shughuli za Elimu kwa michezo;
b) Kubainisha vikwazo vya mawasiliano katika Elimu kwa michezo;
c) Kutumia njia mbalimbali za mawasiliano katika Elimu kwa michezo;
d) Kutaja vifaa vya mawasiliano katika Elimu na Michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

Bungua, majadiliano katika vikundi uwasilishaji, kazi za maktaba, mazoezi kwa vitendo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu na majarida ya Elimu kwa Michezo, magazeti.
b) CD ROM, VCD, DVD, na Projekta yenye mfumo wa sauti.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Insha.
c) Orodha hakiki
d) Mkoba wa kazi

## 2.2 Vyombo vya Habari na Elimu kwa Michezo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana na umuhimu wa vyombo vya habari katika michezo.
b) Kubainisha tofauti ya taarifa rasmi kwa vyombo vya habari na mkutano na vyombo vya habari.
c) Kuandika taarifa rasmi kwa vyombo vya habari.
d) Kuandaa mkutano wa vyombo vya habari.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Igizo dhima.

**Vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu, majarida, vitini na
b) Mifano ya taarifa rasmi kwa vyombo vya habari.
c) Kompyuta na mtandao wa intaneti.
d) CD ROM, VCD, DVD, na projekta.

**Upimaji**

a) Insha.
b) Fomu chunguzi.

## 2.3 Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu kwa Michezo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu kwa Michezo.

b) Kubainisha umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu kwa Michezo.
c) Kutumia vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu kwa Michezo.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Mazoezi kwa vitendo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu, majarida na vipeperushi vya teknolojia ya habari na Mawasiliano.
b) Projecta
c) Mtandao wa internet.

**Upimaji**

a) Jaribio.
b) Kazi binafsi.
c) Fomu ya uchunguzi.
d) Mkoba wa Kazi

## 3.0 USIMAMIZI WA RASILIMALI KATIKA ELIMU KWA MICHEZO

### 3.1 Rasilimali katika Michezo

**Muda: Saa 2**

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya rasilimali katika michezo;
b) Kubainisha aina za rasilimali katika michezo;
c) Kuchambua umuhimu wa rasilimali katika michezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo .
b) Majadiliano ya vikundi.
c) Kisa mafunzo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu mbalimbali vinavyohusu rasilimali watu, vifaa na fedha katika michezo.
b) Majarida ya Utawala na Uongozi katika Elimu kwa Michezo
c) Chati mbalimbali zinazoonesha mgawanyo wa rasilimali na matumizi yake katika michezo.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Kazi binafsi.
c) Insha.

### 3.2 Usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Michezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha mbinu za upatikanaji rasilimaliwatu katika shughuli za michezo;
b) Kutumia rasilimaliwatu katika shughuli za michezo;
c) Kuendeleza rasilimaliwatu katika shughuli za michezo

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi.
b) Kazi za vitendo kazi za maktaba, mswali na majibu.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Video kuonesha mashindano mbalimbali ya michezo.
b) Majarida mbalimbali yanayoonesha rasilimaliwatu katika michezo.
c) Vitabu vinavyohusu rasilimali watu katika michezo.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi jaribio.
b) Fomu ya uchunguzi.
c) Fomu ya uchunguzi
d) Mkoba wa Kazi

### 3.3 Kujitolea katika shughuli za Elimu ya michezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza maana ya kujitolea katika Elimu ya michezo.
b) Kubainisha maeneo muhimu yanayohitaji rasilimali watu wa kujitolea katika tukio la kimichezo.

c) Kuandaa mafunzo kwa rasilimaliwatu wa kujitolea katika elimu kwa michezo.
d) Kukabiliana na tofauti zinazoweza kujitokeza kati ya rasilimaliwatu wa kujitolea katika tukio la kimichezo.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo fikiri kisha shirikisha.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Uwasilishaji wa kutumia video na DVD.
d) Kazi mradi kutathmini mchango wa rasilimaliwatu wa kujitolea kaitka maendeleo ya michezo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu vya utawala na usimamizi wa michezo.
b) Majarida.
c) Video na CD za mashindano mbalimbali.

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Orodha hakiki ya utendaji kazi watu wa kujitolea katika Michezo
c) Insha kuelezea.
d) Fomu ya uchunguzi.
e) Mkoba wa kazi

## 4.0 KUANDAA SHUGHULI ZA ELIMU KWA MICHEZO

### 4.1 Mashindano

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya mashindano.
b) Kusimamia mashindano kwa kuzingatia kanuni za sheria za mashindano husika.
c) Kutathmini mafaniko na mapungufu katika mashindano.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Majadiliano kwa vikundi.
b) Onesho mbinu.
c) Kazi za vikundi.
d) Video zenye matukio mbalimbali ya mashindano.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vipeperushi na majarida.
b) Mifano ya fomu za uamuzi za michezo ya aina mbalimbali
c) Vifaa vya mashindano kwa michezo husika.
d) Mifano ya barua za mialiko.

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Kazi za vikundi.
c) Orodha hakiki.
d) Fomu chunguzi.

## 4.2 Udhamini na Ufadhili katika Elimu kwa Michezo

**Muda**: Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kutofautisha dhana ya udhamini na ufadhili katika elimu kwa michezo.
b) Kubainisha taratibu za kutafuta wadhamini na wafadhili.
c) Kuainisha vipengele vya andiko la udhamini

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Bungua bongo .
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Kualika mtaalam kueleza umuhimu wa dhamini/ufadhili katika michezo.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Vitabu mbalimbali, majarida na vitini vya udhamini na ufadhili;
b) Mtandao wa intanet, kompyuta, laptop. VCD, DVD;
c) Kanda za video na projekta ;
d) Jezi zenye nembo ya mdhamini kwa mfano NMB, ADIDAS, PUMA NA NIKE

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Fomu ya chunguzi.
c) Insha.

## 4.3 Ziara za Kimichezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kubainisha mambo muhimu katika kuandaa ziara za kimichezo.

b) Kuandaa ziara za kimichezo kwa kutumia stadi walizojifunza.
c) Kufanya tathmini ya mafanikio na mapungufu ya ziara ya kimichezo waliyoifanya.

**Mbinu za kufundishia/kujifunzia**

a) Maswali na majibu.
b) Kazi binafsi kuhusu.
c) Kazi mradi.

**Zana/vifaa vya kufundishia na kujifunzia**

a) Chati zinazoonesha mahitaji muhimu katika ziara ya kimichezo.
b) Majarida ya ziara za kimichezo
c) Kisanduku cha huduma ya kwanza.

**Upimaji**

a) Insha.
b) Kazi binafsi.
c) Mkoba wa kazi.

## 5.0 USALAMA KATIKA ELIMU KWA MICHEZO

### 5.1 Usalama wa Vifaa na Mazingira ya Michezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana na umuhimu wa usalama katika michezo.
b) Kubainisha na kuchagua vifaa vya michezo.
c) Kukagua vifaa na viwanja/maeneo ya michezo kabla ya kutumiwa.
d) Kutumia vifaa na viwanja vya michezo kwa usalama wakati wote.
e) Kutunza vifaa vya michezo baada ya kuvitumia.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo fikiri, jozisha na shirikisha.
b) Majadiliano katika.
c) Maswali na majibu.
d) Onyesho mbinu.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Chati ya usalama katika michezo.
b) Kisanduku cha huduma ya kwanza.
c) Vifaa halisi yv michezo mbalimbali.

**Upimaji**

a) Zoezi.
b) Fomu ya uchunguzi.
c) Orodha hakiki.
d) Mkoba wa kazi.

## 5.2 Usalama wa Washiriki katika Michezo

**Muda:** Saa 2

**Malengo Mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza aina anuai za mazoezi yanayofaa kuandaa mwili wa wanafunzi kabla ya kushiriki katika michezo.
b) Kueleza uchezaji unaozingatia kanuni na sheria katika michezo.
c) Kubainisha hatua za kiusalama kwa wanamichezo
d) Kubainisha kanuni za kiusalama kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

**Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji:**

a) Maswali na majibu.
b) Kazi za maktaba.
c) Maswali na majibu.

**Zana/Vifaa vya kufundishia na Kujifunzia**

Vipeperushi Video/filamu zinazoonesha uchezaji salama.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi
b) Fomu ya uchunguzi.
c) Jaribio.

## 5.3 Magonjwa katika Michezo

**Muda:** Saa 3

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini aina mbalimbali za magonjwa katika michezo.
b) Kueleza jinsi magonjwa yanavyoathiri afya ya mwanafunzi katika michezo.
c) Kuainisha magonjwa yanayoweza kukingwa kwa kutumia michezo

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Majadiliano katika vikundi .
c) Kualika mtaalamu kueleza jinsi magonjwa anuai yanavyoweza kukingwa kwa kushiriki katika zoezi na michezo.
d) Maswali na majibu.
e) Kazi mradi .

**Vifaa/Zana za Kufundisha na Kujifunzia**

a) Picha/michoro/chati zinazoonesha waathirika wa magonjwa mbalimbali.
b) Vipeperushi/vitabu/DVDs/CDs/Majarida/Projekta/Video.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi,
b) Jaribio,
c) Fomu ya uchunguzi na
d) Mkoba wa kazi.

## 5.4 Michezo na Ukimwi

**Muda:** Saa 3

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza uhusiano kati ya michezo na mapambano dhidi ya UKIMWI
b) Kuaridhia umuhimu wa waaathirika kushiriki katika michezo

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi na uwasilishaji.
b) Kualika mtaalamu kuaridhia umuhimu wa waathirika katika kushiriki michezo
c) Kazi mradi .

**Vifaa/Zana za Kufundisha na Kujifunzia**

a) Picha/michoro/chati zinazoonesha wachezji maarufu waathirika wa UKIMWI.
b) Vipeperushi .

**Upimaji**

a) Zoezi
b) Jaribio
c) Fomu ya uchunguzi
d) Mkoba wa kazi

## 6.0 AJALI KATIKA ELIMU KWA MICHEZO

### 6.1 Huduma ya Kwanza

**Muda:** Saa 3

**Malengo mahsusi.**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya Huduma ya Kwanza.
b) Kueleza umuhimu wa Huduma ya Kwanza katika michezo
c) Kubainisha vifaa vilivyomo ndani ya kisanduku cha Huduma ya Kwanza.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Bungua bongo.
b) Fikiri, jozisha na shirikisha.
c) Majadiliano katika vikundi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kisanduku cha Huduma ya Kwanza.
b) Picha/mchoro unaoonesha Kisanduku cha huduma ya kwanza na vifaa vyake.

**Mbinu za Upimaji**

a) Maswali mafupi kueleza.
b) Orodha hakiki na Fomu ya uchunguzi.

### 6.2 Utoaji wa Huduma ya Kwanza katika Michezo

**Muda: Saa 3**

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya ajali michezoni

b) Kuchambua aina mbalimbali za ajali michezoni na vyanzo vyake
c) Kubainisha njia mbalimbali za utoaji wa huduma ya kwanza.
d) Kuonesha jinsi ya utoaji wa huduma ya kwanza kwa mwanafunzi aliyeumia michezoni.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Kazi za maktaba.
b) Majadiliano katika vikundi.
c) Maswali na majibu.
d) Onyesho mbinu na kazi mradi.

**Vifaa/Zana za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Michoro/picha/chati zenye kuonesha aina mbalimbali za ajali michezoni
b) Video/filamu.
c) Kisanduku cha huduma ya kwanza
d) Video/DVDs/ zenye kuonesha watu wakitoa huduma ya kwanza kwa ajali mbalimbali michezoni.
e) Machela, magango, barafu.

**Mbinu za Upimaji**

a) Maswali mafupi .
b) Fomu ya uchunguzi.

### 6.3 Mazoezi kwa Majeruhi

**Muda:** Saa 1

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kubaini aina mbalimbali za mazoezi sahihi kwa majeruhi.
b) Kusimamia mazoezi kwa majeruhi.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Majadiliano katika vikundi kazi za maktaba, kazi mradi.
b) Kumwalika mtaalamu kufundisha mazoezi kwa majeruhi.
c) Igizo dhima.

**Zana/vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Michoro/picha/chati zinazoonesha mazoezi mbalimbali kwa majeruhi
b) Video na filamu zinazoonesha aina mbalimbali za majeruhi wakifanya mazoezi.

**Upimaji**

a) Maswali mafupi.
b) Jaribio mkoba wa kazi ya fomu ya uchunguzi, fomu ya mlinganisho wa viwango.

## 6.4 Matumizi ya Madawa Katika Michezo

**Muda:** Saa 3

**Malengo mahsusi**

Baada ya kukamilisha mada ndogo hii, mwanachuo aweze:-

a) Kueleza dhana ya madawa katika michezo.
b) Kubainisha aina za madawa zinazotumika katika katika michezo
c) Kuchambua matumizi mbalimbali ya madawa, katika michezo
d) Kubainisha madawa yanayozuiliwa kutumiwa katika michezo na athari zake.

**Mbinu za Kufundishia na Kujifunzia**

a) Maswali na majibu kazi za maktaba.
b) Fikiri, jozisha na shirikisha.
c) Majadiliano katika vikundi.
d) Kazi mradi.

**Zana/Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia**

a) Michoro/picha/chati zinazoonesha aina mbalimbali za madawa, watu walioathirika na madawa.
b) Vipeperushi/vijarida vinavyoonesha madhara ya matumizi mabaya ya madawa katika michezo.

**Upimaji**

a) Orodha hakiki kubainisha aina za madawa katika michezo.
b) Insha, zoezi kuchambua matumizi ya madawa katika michezo na athari zake.
c) Jaribio kuhusu madawa katika michezo, Fomu za ulinganifu wa viwango.

## REJEA


Chappelet, J. ( 2002). **Strategic and Performance Management of Olympic Sport Organisations.** Champaign: Human Kinetics.

Chelladurai, P. (2001). **Managing Organizations for Sport and Physical Activity: A systems Perspective.** Arizona: Holcomb Hathaway, Publisher.

Chelladurai, P. and Madella, A. (2006). **Human Resource Management in Olympic Sport Organisations.** Champaign: Human Kinetics

Davis, K. A. (1994). **Sport Management: Successful Private Sector Business Strategies.** Madison: Brown and Bandmark.

Ferraud, A. and Torrigiani L (2005). **Marketing of Olympic Sport Organisations. Auckland:** Human Kinetics.

Getshell, B. (1979). **Physical Fitness a way of Life**. 2nd ed. John Wiley and Sons.

Hernandez, R. A. (2002). **Managing Sport Organizations.** Auckland: Human Kinetics.

International Olympic Committee (2001). **Sport Administration Manual.** Laussanne: Hurford enterprises.

Reilly, T. Ed (1981). Sport Fitness and Sports Injuries. Faber and Faber limited. London.

Siedentop, D. (2001). **Introduction to Physical Education, Fitness and Sport.** London: Mayfield Publishing Company.

Stotlar, D. K. (2001). **Developing Successful Sport Sponsorship Plans.** Morgantown: Fitness Information Technology.